

**HOTUBA YA MWENYEKITI WA BODI YA WAKURUGENZI YA  
MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO WAKATI WA UZINDUZI WA BODI  
HIYO TAREHE 25 NOVEMBA, 2022 KATIKA UKUMBI WA OFISI ZA  
MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO, GHOROFA YA NNE, JENGO LA  
UTUMISHI, JIJINI DAR ES SALAAM**

---

**Mheshimiwa Jenista Mhagama (MB):** *Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,  
Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,*

*Dkt Laurean J. P Ndumbaro: Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya  
Utumishi wa Umma na Utawala Bora,*

*Wajumbe Wateule: Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao,*

*Eng. Benedict Ndomba: Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali  
Mtandao, Menejimenti ya Mamlaka ya Serikali  
Mtandao,*

*Waandishi wa Habari,*

*Mabibi na Mabwana,*

*Nawasalimu Kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,*

**Mheshimiwa Waziri,**

Awali ya yote ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema, na kutuwezesha kukutana hapa leo hii. Hakika hii ni siku muhimu kwetu sisi kushuhudia uzinduzi wa Bodi yetu, ili hatimaye kukabidhiwa rasmi majukumu ya kusimamia Taasisi hii muhimu katika utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao kwa ajili ya kuboresha utendeji kazi katika taasisi za umma na utoaji wa huduma kwa Umma.

**Mheshimiwa Waziri,**

Kwa niamba ya Wajumbe wa Bodi nikushukuru wewe binafsi kwa kutenga muda wako ili kuzindua Bodi hii, huku tukitambua majukumu mazito ya Kitaifa uliyonayo. Pili, binafsi namshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mheshimiwa** . Samia Suluhu Hassan, kwa kuniamini na kuiteua kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi hii nyeti iliyoanzishwa kwa ajili ya kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali Mtandao pamoja na kuhimiza uzingatiaji wa sera, sheria, kanuni, viwango na miongozo ya Serikali Mtandao katika taasisi za umma, kwa ajili ya kuhakikisha kuwa taasisi za umma zinatumia TEHAMA kwa usahihi ili kufikia malengo kusudiwa.

**Mheshimiwa Waziri,**

Kwa pamoja tumepokea majukumu, maelekezo na changamoto, ambapo tunakuhakikishia kuwa tutajitahidi kadri ya uwezo na weledi wetu kuisimamia na kuiongoza Mamlaka ya Serikali Mtandao, kupitia Menejimenti na Watumishi wake, katika kutekeleza majukumu iliyokasimiwa.

**Mheshimiwa Waziri,**

Tunaahidi kuwa tutatoa ushirikiano kwa Wizara na kwako wewe binafsi, ikiwemo kujitahidi kadri ya uwezo wetu kuyaelewa malengo ya uwepo wa Taasisi hii, ili kuhakikisha kuwa Serikali na Umma unapata manufaa kutokana na uwekezaji uliofanyika katika utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao. Tumepokea Nyaraka, ambazo ni vitendea kazi vyetu, tutazitafsiri na kusimamia utekelezaji wake kwa vitendo.

**Mheshimiwa Waziri,**

Kwa mara nyingine nikushukuru kwa kuizindua Bodi yetu.

**Ahsanteni kwa Kunisikiliza**